

## **Je, Sisi Ni Makuhani Wa Mungu?**

Mimi ni kuhani. Wewe ni kuhani kama umezaliwa tena katika ufalme wa Mungu. Kwa hiyo kama tumezaliwa tena basi sisi wote ni makuhani katika ufalme wa Mungu na Yesu Kristo ndiye Kuhani Mkuu. Kwa hiyo Biblia inatufundisha wazi kwamba wakristo wote ni makuhani. Lakini baada ya kufunguliwa ufalme wa Mungu watu walianza kufundisha kwamba kuna wakubwa tu ambayo ni makuhani. Ndiyo maana leo katika madhehebu mbali mbali wanao Makuhani na washiriki tu wa kawaida. Na wanamini ndiyo kazi tu ya Mkuhani kutoa “Sakramenti” kwa Mungu. Lakini tutaangalia leo, Makuhani ni nani na Kazi yao ni nini?

### **Kuhani ni Nini?**

Neno “Kuhani” katika Agano Jipya lina maana mtoto wa mfalme au mtumishi. Na makuhani wote kwenye maandiko ni lazima wawe na madhabahu na ni lazima watoe sadaka. Na hakuna mtu kwenye maandiko alikuwa na uwezo wa kutoa sadaka kwa ajili ya watu mbele ya Mungu. Ndiyo Manabii wengi wametoa sadaka, lakini kazi ya manabii ni kutumikia Mungu kwa ajili ya watu. Lakini kazi ya Kuhani ni kutumikia Watu mbele ya Mungu. Kwa tofauti ipo. Na hata leo kama wewe ni kuhani ni lazima utoe matoleo na sadaka kwa Mungu.

### **Kuhani Wetu Leo Kama Kanisa.**

Hatuwezi kusoma kuhusu Ukuhani wa Yesu mpaka kitabu cha Waebrania katika Agano Jipya. Na hapa mwandishi anamtukuza yeye kama Kuhani Mkuu wa pekee na wa milele. Yeye tu ni Kuhani Mkuu wetu na hakuna mwingine. Amekwisha mwaga damu yake kwa ajili yetu na damu yake yanafaa milele. Lakini Ukuhani wetu umetajwa kidogo sana katika kitabu cha Waebrania. Ni Ebr. 10:22 inafundisha sisi jinsi tunavyokuwa Makuhani. Na Ebr. 13:15-16, inatufundisha tunahitaji kutoa matoleo gani kwa Mungu.

### **Waebrania 13:15-16.**

Hapa tunaona mwandishi wa kitabu hiki anaongea kuhusu kazi ya Mkristo ambaye ni kazi ya kuhani tena. Kwa hiyo tunaona hapa kwamba sio Makuhani walionahaki ya kutoa sadaka kwa Mungu. Sio sadaka ya Wanyama bali sadaka Mungu anayohitaji siku hizi.

### **1 Pet. 2:5-9.**

Petro katika barua hii anaongea na Wakristo waliotawnyika sana. Na katika mstari wa tano Petro anasema ninyi nanyi? \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_ . Alikuwa ana onyesha Wakristo wa leo wanayotakiwa kuachana na dunia na kwa hiyo Wakristo sio Hekalu tu (1 Kor. 6:16-20) bali ni makuhani katika miili yao. Tena katika mstari wa tisa aliongeza kwamba sisi ni “Ukuhani wa kifalme”. Alikuwa na tukuzwa hali yetu ya kiroho na uhusiano wetu na Mungu. Na leo kwa sababu sisi ni Makuhani basi ni lazima tutoa matoleo au sadaka kama Mungu

anavyotaka leo na ni laimza tukumbuke kuwa ni Makuhani tu walioamriwa kutoa sadaka. Na kama Makuhani au watu wa Mungu sisi ni mali yake, na kama tu mali yake tunakaribia kiti cha ufalme wake kupitia Kuhani Mkuu Yesu Kristo, 1 Tim. 2:5.

### **Ufunuo 1:6.**

Yohana mtume aliyependwa sana na Yesu anakumbusha sisi katika mstari huu kwamba Kristo alitufanya sisi, “Kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu.” Kwa jumla sisi wote ni Ufalme wake lakini peke yetu kila moja ni kuhani katika Ufalme wake. Ndiyo, Yohana mwenyewe alitufundisha sisi kuwa ni makuhani mbele za Mungu. Hakusema walikuwa wachache ndani ya Kanisa ambao ni Makuhani lakini ni sisi wote, tena alirudia maneno yale yale katika 5:10.

### **Warumi 12:1.**

Angalia maneno machache hapa: “Ndugu...Dhabihu...Ndiyo ibada yenu yenye maana.” Ndugu sio watu waliochagulia na kusoma shule fulani walikuwa na kutoa dhabihu au ibada yenye maana. Ni Wakristo wote! Kwa sababu tunajua Makuhani tu wanaweza kutoa sadaka katika Agano Jipya, mstari huu unaonyesha ndugu ni makuhani na ni lazima tutii mstari huu. Kwa hiyo ni lazima tushukuru tu kwamba sisi wote ni makuhani na hatuhitaji kupitia mtu au mwanadamu ye yote ilitufike kwa Mungu. Ni kupitia Yesu tu.

### **Matoleo au Sadaka ya Kuhani ni Nini Leo?**

Tumesoma sehemu nyingi, tayari tumeona kazi nyingi ya kuhani siku hizi chini ya Agano Jipya. Kwa hiyo tuangalie oradha ya kazi tunayoweza kufanya kazi zile ni kama sadaka kwa Mungu.

**Imani yetu ni Sadaka.**

**Upendo wa Mungu si Sadaka wetu.**

**Kutubu kwetu ni Sadaka.**

**Kukiri imani katika Yesu Kristo ni Sadaka.**

**Kubatizwa katika Kristo ni Sadaka.**

**Kumsifu Mungu ni Sadaka.**

**Kutoa ni Sadaka.**

**Kuimba ni kutoa Sadaka.**

**Kuomba ni kutoa Sadaka.**

**Maisha ya kumshima Mungu na kumpenda ni sehemu ya maisha yetu na tena ni Sadaka.**

### **Hitimisho:**

Kwa matoleo ya juu Mungu anashukuru sana kama tunatoa kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Kwa hiyo tunaweza kutoa sadaka kwa sababu sisi ni Makuhani wa Mungu.